Somo la Ziada: Kwa Wachungaji

Lengo Kuu
Kuna hadithi nyingi za Biblia ambazo zitawasaidia waumini kukua katika imani yao.

Utangulizi

Hadithi zote katika Biblia zinaweza kutufundisha kuhusu Mungu na kuwasaidia waumini kukua katika imani yao. Somo hili litakufundisha jinsi ya kutayarisha mahubiri kwa kutumia hadithi za Biblia. Pia inapendekeza hadithi 20 za Biblia unazoweza kuanza kufundisha mara moja. Kila hadithi inaonyesha ukweli muhimu kuhusu Mungu ni nani na uhusiano wetu naye.

Ikiwa huna Biblia yako mwenyewe, uwe pamoja na mchungaji mwingine aliye nayo. Fanya kazi nao kugeuza kila kifungu kuwa hadithi na kukikariri. Kisha unaweza kusimulia hadithi hiyo katika ushirika wako.

Jinsi ya Kutayarisha Mahubiri kwa kutumia Hadithi za Biblia

Hatua za kutayarisha / kuandaa hadithi

1. Ielewe hadithi.
   Soma hadithi hiyo katika Biblia. Fikiria kuhusu hadithi.
   i. Inakufundisha nini?
   ii. Wazo kuu ni lipi?
   iii. Kwa nini hadithi hii iliwekwa kwenye Biblia?
2. Vuta taswira ya hadithi.
   Fikiria ulikuwa mmoja wa wahusika. Chukua muda kujifikiria kama wahusika wakuu wote. Ungejisikiaje? (Kwa mfano, ungekuwa unasimulia hadithi ya wageni waliokuja kumwambia Abrahamu na Sara kwamba baada ya mwaka mmoja wangekuwa na mtoto. Abrahamu angejisikiaje katika hadithi hiyo? Sara angejisikiaje?)
3. Sema hadithi kwa sauti.
   Unaweza kusimulia hadithi kwa mtu yeyote – mwenzi wako, mtoto, au rafiki. Kusimulia hadithi kwa sauti hukusaidia kufikiria juu ya kile unachotaka kukisema. MAra baada ya kusimulia hadithi mara chache unaweza kuiandika au kuirekodi ikiwa njia hiyo itakusaidia kuikumbuka vyema.
4. Jaribu kuweka mazungumzo ya majibizano.
   Mazungumzo ya majibizano hufanya hadithi kuvutia zaidi. (Kwa mfano, ukisimulia hadithi ya bustani ya Edeni na nyoka, hakikisha kwamba unajumuisha maneno halisi ambayo nyoka alimwambia Hawa.)
5. Eleza kwa nini hadithi ni ya muhimu na inafundisha nini kuhusu Mungu na watu.
   Kwa hadithi za Biblia tunazotoa katika somo hili, tutakupa baadhi ya mambo ya kueleza.
6. Toa njia ambazo tunaweza kutumia hii katika maisha yetu
   Watu wanahitaji kutumia kile wanachojifunza, au hakitakuwa sehemu yao na tabia zao. Yakobo 1:22-25 inasema, ‘Msisikilize neno tu, na hivyo mkijidanganya nafsi zenu. Fanya inavyosema. Yeyote anayesikiliza neno lakini hafanyi linavyosema, ni kama mtu anayejitazama uso wake kwenye kioo, na baada ya kujitazama, huenda na mara moja anasahau jinsi anavyofanana. Lakini

mtu yeyote anayetazama kwa makini sheria kamilifu iletayo uhuru, na kudumu humo, bila kusahau yale aliyosikia, bali anayafanya, atabarikiwa katika yale anayofanya.

Hadithi 20 za Biblia za Kufundisha

Katika Moduli ya 1 ulijifunza hadithi ya Uumbaji na Anguko. Katika Moduli ya Uinjilisti somo la 8 ulifanya mazoezi ya kusimulia hadithi hii kutoka Mwanzo 1-2. Hadithi hii inaeleza kwamba Mungu aliumba kila kitu. Inafundisha kwamba dhambi ya mwanadamu ndiyo sababu ya kuvunjika kwa ulimwengu. Hapa kuna hadithi zaidi za kufundisha, na baadhi ya mambo muhimu unayoweza kuyapata kutoka kwenye hadithi hizo.

AHADI YA MUNGU KWA ABRAHAMU

Mwanzo 12:1-9, Mwanzo 15

- Mungu alimchagua Abrahimu kwa sababu Abrahimu alimwamini, si kwa sababu ya jambo lolote alilolifanya Abrahimu.
- Ahadi za Mungu hazitutegemei sisi, bali tabia yake, ambayo haibadiliki kamwe.

ABRAHAMU NA ISAKA

Mwanzo 22:1-19

- Abrahamu alichagua kumwamini Mungu kwa jambo alilolijali zaidi.
- Mungu hutupatia kila kitu tunachohitaji.

YUSUFU

Mwanzo 37-45

- Mungu hutumia hata mapambano ya kutisha na yenye maumivu kwa ajili ya mpango wake.
- Mungu anajua wakati ujao na anatawala kila kitu.

MUSA NA KUTOKA

Kutoka 5-14

- Mungu ana nguvu kuliko miungu mingine yote. Anatawala dunia.
- Mungu aliwasikia watu wake.
- Mungu hutimiza ahadi zake.

JANGWANI

Kutoka 16, 17:1-7

- Mungu alitoa kila kitu ambacho watu wake walihitaji. Kwa Mungu, rasilimali hazina ukomo.
- Mungu huwaongoza watu wake.

UTOAJI WA SHERIA

Kutoka 20-21

- Mungu anajali kila eneo la maisha.
- Kusudi la Mungu kwetu ni jema.
- Watu hawakuweza kushika sheria. Sote tunamhitaji Mwokozi.

VITA YA YERIKO

Yoshua 6:1-21

- Mungu hupigana vita vyetu tunapomwamini.

- Lazima tutii hata kama haileti maana kwetu.

DAUDI NA GOLIATHI
1 Samweli 17:1-50
- Mungu anaweza kumtumia yeyote anayemwamini.
- Tukiwa na Mungu, tutashinda. Hakuna haja ya kuogopa.

YONA NA SAMAKI MKUBWA
Yona 1-3
- Mungu ana huruma kwa watu wote.
- Tunapotubu, Mungu hutusamehe.

ELIYA NA MANABII WA BAALI
1 Wafalme 18:16-40
- Ukimwabudu Mungu, huwezi kuabudu kitu kingine chochote. Kila mtu lazima achague kati ya Mungu na sanamu.
- Mungu wetu ana nguvu kuliko roho na 'miungu' yote.

TANURU LA MOTO
Danieli 3
- Mungu anaweza kutusaidia katika hali yoyote. Ana nguvu zaidi kuliko watawala wa kidunia.
- Hata kama Mungu hafanyi tunachotaka, tunaweza kumwamini na kumtii.

HADITHI YA KRISMASI
Luka 1:26-38, Luka 2:1-21
- Yesu ni mwanadamu kamili na ni Mungu kamili (sio mtu wa pekee tu, wala si Mungu aliyejigeuza kama mwanadamu).
- Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa, aliyezaliwa ili kutuokoa kutoka kwenye dhambi.

YESU UTULIZA DHORUBA
Luka 8:22-25
- Yesu ana nguvu juu ya vitu vyote.

YESU AMPONYA MTU MWENYE PEPO
Luka 8: 26-39
- Yesu ana uwezo juu ya roho zote.

YESU ANASIMULIA HADITHI MBILI – SARAFU ILIYOPOTEA NA KONDOO ALIYEPOTEA
Luka 15:1-10
- Kila mtu ni wa thamani kwa Mungu.
- Mungu anataka kila mtu atubu na kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu.

YESU ANAMFUFUA LAZARO KUTOKA WAFU
Yohana 11:1-43
- Yesu ana uwezo juu ya kifo.
- Yesu anatujali sana hata anahuzunika tunapokuwa na huzuni.

KARAMU YA MWISHO

Luka 22:14-20

- Yesu ni Mungu, lakini alikuja kutumikia.
- Lazima tuhudumiane sisi kwa sisi pia.

KUSULUBIWA NA KUFUFUKA

Luka 23:13-56, Mathayo 28:1-10

- Yesu alikufa kwa ajili yetu. Alichukua dhambi zetu na adhabu ya kifo juu yake mwenyewe.
- Yesu ana nguvu kuliko mauti; hakuna haja ya kuogopa kifo.

PENTEKOSTE

Matendo ya Mitume 2:1-12

- Yesu aliporudi mbinguni, alimtuma Roho Mtakatifu akae ndani yetu.
- Roho Mtakatifu hutupatia uwezo wa kuishi kama Mungu anavyokusudia.

UONGOFU WA PAULO

Matendo ya Mitume 22:1-21

- Tunaokolewa kwa neema, si kwa matendo (Paulo alikuwa Mfarisayo).
- Injili ni ya kila mtu.